

# JINSI YA KUTUMIA HUDUMA ZETU

rtd-denver.com | 303.299.6000 | customercare@rtd-denver.com

Kama mtoaji wa huduma za usafiri wa umma kwa eneo la kati la Jiji la Denver, RTD inaunganisha jumuiya kwa mabasi, treni, Access-a-Ride (huduma kwa watu wenye ulemavu), usafiri wa masafa mafupi mitaani kama vile FlexRide, na zaidi. Iache RTD ikusaidie kutimiza mahitaji yako ya usafiri!

## MIPANGO YA VIPUNGUZO VYA NAULI

Huenda wewe na familia yako mnastahili vipunguzo. Vipunguzo vya nauli vinatolewa kwa:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Watu walio na mapato ya chini** | **Wakongwe** (miaka 65+) | **Watu walio na ulemavu** | **Vijana** (maiaka 19 kwenda chini)* |

**Jifunze zaidi kuhusu ustahiki na kujaza vipunguzo vya nauli kupitia rtd-denver.com/discount-fares!**

*Vijana walio na miaka 19 au chini ya hapo wanasafiri bila gharama kwa msaada wa mpango wa Kutotoza Vijana Nauli (Zero Fare for Youth).

## JINSI YA KUNUNUA TIKITI NA PASI

Iwe unasafiri kwa basi au treni, ni rahisi kununua tikiti au pasi zako za RTD. Chagua nauli ambayo inatimiza mahitaji yako (saa 3, Kila siku, au kwa Mwezi), na utakuwa sawa.

### Utanunua wapi Tikiti na Pasi

- Machine za kuuza tikiti kwenye vituo vyote vya treni
- Mhudumu wa basi (ikiwa unalipa pesa taslimu, lipa kiasi kamili)
- Kupitia rtdonlinestore.com
- Maduka ya mauzo ya RTD
- Maduka ya King Soopers na Safeway yanayoshiriki




### RTD kwenye Simu mahiri yako

Njia rahisi zaidi ya kununua tikiti ni kwenye simu mahiri yako. Changanua msimbo wa QR ulio kulia ili kupakua programu ya **RTD MyRide** kwa IOS au Android.

**Talii huduma za RTD, panga safari yako, na zaidi kupitia rtd-denver.com.**

# PANGA SAFARI YAKO

Tumia kifaa cha RTD **Next Ride** (app.rtd-denver.com/nextride) kupanga safari yako kuanzia mwanzo hadi mwisho, kuangalia basi au treni yako inavyoendelea, au kuangalia ucheleweshaji au kubatilishwa kwa wakati halisi.

# TUMIA BASI

**Vidokezo muhimu**

- Fika kwenye kituo mapema.
- Basi linapofika, angalia ishara ya kidijitali kwenye sehemu ya juu ya mbele kwenye basi kuhakikisha njia na mahali unahitaji kwenda!
- Abiri basi na ulipe nauli yako kwa kiasi taslimu, tikiti inayostahiki, pasi, kadi ya MyRide au tikiti ya kidijitali.
- Ikiwa unatumia kadi ya MyRide au tikiti ya kidijitali, ichanganue kwa kutumia kithibitishaji.
- Unapoelekea kufika mahali unakoenda, vuta kamba ya manjano, au ubofye kitufe kuomba basi kusimama.
- Shuka kupitia mlango wa nyuma inapowezekana.



# ABIRI TRENI

**Vidokezo muhimu**

- Fika kwenye kituo. Angalia ishara za kidijitali au Safari Inayofuata ujue treni inayofuata.
- Nunua tikiti au pasi kwenye mashine ya kuuza, au uwe na tikiti yako ya kidijitali au pasi tayari kabla ya kuabiri.
- Thibitisha tikiti iliyochapishwa kwenye mashine nyekundu za "V", kadi yako ya MyRide kwenye vithibitishaji vyeusi na vya fedha, au uwezeshe tikiti yako ya kidijitali. Hauhitajiki kuthibitisha tikiti unazonunua kutoka kwa mashine za kuuza tikiti.
- Simama nyuma ya mstari wa manjano ili kusubiri treni.
- Angalia ishara ya kidijitali au usikilize tangazo ili ujue unapokaribia eneo unakokwenda.



# KUWA SALAMA KWENYE MABASI NA TRENI




Ikiwa utaona kitu, sema jambo. Changanua msimbo wa QR ulio kushoto uweze kupakua programu ya RTD **Transit Watch** ili kuripoti shauku za usalama kwenye au karibu na mfumo wa RTD. Pia unaweza kupiga simu kwa 303.299.2911 au kutuma ujumbe mfupi kwa 303.424.9100 kuripoti shauku za kiusalama. Tembelea rtd-denver.com/transitwatch ujifunze mengi zaidi.

# MSAADA NA USAIDIZI WA LUGHA

Piga simu kwa Huduma kwa Wateja kupitia 303.299.6000 ukiwa na maswali yoyote kuhusu RTD. Huduma za ukalimani zinapatikana bila gharama katika zaidi ya lugha 200. Kwa lugha ya Kihispania, bonyeza 2. Kwa lugha nyingine zote, bonyeza 8, kisha mwambie wakala lugha unayotumia na usalie kwenye simu hadi akuunganishe na mkalimani.

**Talii huduma za RTD, panga safari yako, na zaidi kupitia rtd-denver.com.**